
1

Jinsi ya Kuboresha Elimu:
Mafunzo Kutoka Jumuiya Nne



Jinsi ya Kuboresha Elimu: Mafunzo Kutoka Jumuiya Nne ni kitabu cha kwanza katika vitabu viwili vya kujifunza mfululizo wa ufahamu katika masomo. Kitabu hiki kinatokana na taarifa zilizokusanywa na HakiElimu kupitia Mpango wa Utawala wa Jamii katika wilaya nne ambazo ni Serengeti, Mwanza, Misungwi na Ukerewe. Mpango huo uliwezesha jumuiya mbalimbali wakiwepo walimu, wazazi na wanafunzi kuleta mabadiliko mashuleni na kushawishi utoaji wa maamuzi kwa kuwezesha ushiriki wao kwenye utawala wa shule. Mafunzo haya yalikusanywa katika wilaya hizi mwaka 2002 na 2003. Dhana kuu katika zoezi zima la mkusanyo huu ilikuwa ni usikivu makini. Mpango wa Utawala wa Jamii ulifanywa mwaka 2005. Mafunzo haya yanaweza kuwatia moyo watu na jumuiya mbalimbali Tanzania kuhakikisha kuwa watoto wote wanapata elimu safi na bora.



HakiElimu inafanya kazi kufikia usawa, ubora, haki za binadamu na demokrasia katika elimu kwa kuwezesha jamii kubadili shule na mfumo wa uundaji wa sera za elimu, kuchochea mijadala yenye ubunifu na kuleta mabadiliko, kufanya utafiti yakinifu, kudadisi, kufanya uchambuzi na utetezi na kushirikiana na wadau kuendeleza manufaa ya pamoja na haki za jamii.

S.L.P. 79401 • Dar es Salaam • Tanzania
Simu: (255 22) 2151852 au 3 • Faksi: (255 22) 2152449
info@hakielimu.org • www.hakielimu.org

Jinsi ya Kuboresha Elimu:

Mafunzo Kutoka Mpango wa Utawala wa Jamii wa HakiElimu 2002-2003

Waandishi:	Japhet Makongo na Khalid Peter
Wachangiaji:	Veena Gokhale, Pius Makomelelo, James Mikenze, Filbert Kapela, Maketu Nyamwero & Emmanuel Mbaga
Wahariri:	Krista Riber, Godfrey Telli, Fausta Musokwa na Richard Lucas
Mhariri Mkuu:	Rakesh Rajani

© HakiElimu 2005
SLP 79401, Dar es Salaam, Tanzania,
Simu: (255 22) 2151852/3 Faksi: (255 22) 2152449
Info@hakielimu.org www.hakielimu.org

ISBN 9987-423-42-6

Sehemu yoyote ya kitabu hiki inaweza kuchapishwa kwa madhumuni yasiyokuwa ya kibiashara; ili mradi tu itajwe kuwa imetolewa wapi, pia nakala mbili za toleo hilo zipelekwe HakiElimu.

YALIYOMO

Utangulizi:..... i

1. Muziki na Michezo ni Muhimu Katika Elimu…….. 1

2. Maendeleo Yaleta Utata?..... 3

3. Kwenda Shuleni Pamoja na Simba……..... 5

4. Fedha Zilizoahidiwa Hazifiki Shuleni…….. 7

5. Mbao za Matangazo Zaleta Mafanikio…….. 8

6. Elimu Bora Dhidi ya Mahari……..... 9

7. Mawazo ya Mwalimu Yaibadili Shule……. 11

8. “Majalada” Yapotea Siku ya Malipo……... 13

9. Wanafunzi Wataka Kujua Taratibu ……..... 15

10. Maktaba Huhamasisha Kujifunza……... 17

11. Kutoa Majibu Yasiyo Sahihi kwa Makusudi……... 19

12. Mwanafunzi Atia Saini Kwenye Hundi za Shule. ……..... 21

Utangulizi

Kijitabu hiki kimeandaliwa kwa kutumia taarifa zilizokusanywa kutoka kwenye programu ya Utawala wa Jamii ya HakiElimu katika wilaya nne: Serengeti, Mwanza, Misungwi na Ukerewe. Programu hii iliwezesha jamii - ikiwa ni pamoja na walimu, wanafunzi na wazazi – kuleta mabadiliko shuleni na kushawishi utoaji wa maamuzi, kwa kuwezesha kushiriki kikamilifu kwenye utawala wa shule.

Lengo kuu lilikuwa ni kutoa msukumo wa kidemokrasia kwenye kamati za shule, na kuchochea makundi yaliyosahauliwa kihistoria kushiriki pamoja kuleta mabadiliko. Wanafunzi na walimu walihimizwa kujiunga na vyama vilivyokuwepo, na kuunda vya kwao. Programu hii iliwahimiza wananchi kupeana taarifa na kuchukua hatua za pamoja kuboresha elimu kwenye jamii zao.


Ni muhimu kuelewa undani wa misukumo na tamaduni za kila jamii. Mara nyingi, kitu ambacho ni cha muhimu kwa wanakijiji wa Mbalibali, kinaweza kutoonekana hivyo na wengine, na hivyo kusababisha juhudi za kuleta mabadiliko kushindikana. Na huenda tukashindwa kuelewa kwa nini tumeshindwa. Jibu linabaki, japo kwa kiasi fulani tu, katika kusikilizana.

Kijitabu hiki kinawasilisha changamoto zinazokumba elimu na demokrasia katika wilaya hizi nne. Mafunzo haya yalikusanywa toka kwa walimu na wanafunzi, wa shule za wilaya hizi mwaka 2002 na 2003. Tumebainisha au kutambua hatua zilizofanikiwa na ambazo hazikufanikiwa kwa sababu moja au nyingine. Kila moja ya mifano hii 12 inayowasilishwa hapa inatoa somo la namna ya kuboresha elimu. Baadhi ya mambo yanabadilika kutokana na hatua wanazochukua wananchi na majukumu yao kwa ujumla. Mafunzo haya yamepatikana kwa kuwasikiliza wananchi, wakiwemo wazazi.

Majina ya watu walionukuliwa yamebadilishwa ili kuficha utambulisho wao. Ofisi za HakiElimu wilayani zilifungwa katikati ya mwaka 2005. Programu ya Utawala wa Jamii itaendelezwa na wananchi wenyewe, kwa msaada wa serikali za mitaa. Mafundisho haya yanatoa ushahidi wa mafanikio ya wananchi na yanaweza yakatumika kuchochea jamii nyingine za Tanzania.

1 Muziki na Michezo ni Muhimu katika Elimu

Bwana Julius Mahandeka, Mwalimu Mkuu, alipewa uhamisho kwenda shule ya Msumi Kahama. Mara moja alibaini kwamba wanafunzi hawakuwa na ari na shule. Walimu nao hawakujali, na hakukuwa na hatua za pamoja za kubadili hali hiyo. Jumuia nzima ilionesha kutojali ustawi wa shule. Mwalimu Mahendeka alikuta kwamba katika darasa la saba, wanafunzi 9 tu ndio waliohudhuria



darasani pia mahudhurio kwa ujumla yalikuwa asilimia 45 na idadi ya watoro ilikuwa kubwa. Katika miaka 5 iliyopita hakukuwa na hata mwanafunzi mmoja aliyechaguliwa kuingia shule ya sekondari. Karibu kila mara shule hiyo ilikuwa ya mwisho katika matokeo ya shule za msingi katika Mkoa wa Mwanza. Ni dhahiri kwamba kuwa kulikuwa na tatizo na mwalimu Mahendeka alidhamiria kulishughulikia.

Aliishauri kamati ya shule kuwekeza katika kununua vifaa vya michezo na muziki ili kuwavutia wanafunzi.

Shule ilinunua vifaa vya bendi ya shule pamoja na vya michezo ikiwemo mipira ya miguu na ya pete kwa kutumia pesa kidogo ya ruzuku waliyopewa na shirika lisilo

la kiserikali la HakiElimu. Ratiba ya shule ilipangwa upya ili kutoa mwanya wa muziki na michezo. “Bendi ilipocheza kwa mara ya kwanza wanakijiji wengi walikuja shuleni kuona nini kilichokuwa kinandelea. Hata baadhi ya watoto ambao hawakuwa shuleni walikuwa miongoni mwao. Nilistaajabu pale nilipoona watoto hao wakijiunga na gwaride la wanafunzi. Baada ya gwaride hawakurudi nyumbani bali madarasani kwao ingawa hawakuwa na sare za shule,” anasema Bwana Mahendeka.

Bendi ilijenga upya motisha miongoni mwa wanajamii. Sasa wazazi wana ari ya kujihusisha na masuala ya shule. Wanafunzi wamejenga mtazamo mzuri kwa kazi zao mahudhurio yameongezeka sana kutoka 45% mnamo 2002, kufikia 75% mwaka 2003.

Bwana Mahendeka ameleta badiliko rahisi lakini lenye nguvu katika jamii yake. Masomo wayapatayo darasani watoto ni muhimu lakini hiyo haitoshi. Watoto wanahitaji kujishughulisha; wanahitaji kujifurahisha na pia mazoezi ya viungo yana manufaa kwao.

Mwalimu Mahendeka anasema kwamba shule ya Msingi Kahama ina mpango wa kudhihirisha uwezo wake kwa mara ya kwanza katika mitihani ya Taifa.

2 Maendeleo Yaleta Utata

Walimu katika Wilaya ya Serengeti, hawajui wafanye nini. Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), umeanzisha masomo mapya, umebadili mtaala na mitihani na kuhimiza njia mpya za ufundishaji. Pia wameanza kujenga madarasa na vyoo vipya. Lakini inaelekea wamesahau sehemu muhimu kuliko zote ya mpango huu.

"Wala hatukumbuki mara ya mwisho ilikuwa lini tulipoitwa kwa ajili ya mafunzo kazini. Tunafundisha kutokana na uzoefu si kwa ujuzi, hatuna uhakika kama tunachukua njia sahihi serikali inapaswa ijue kwamba huu ukosefu wa mafunzo utawaathiri vibaya wanafunzi" anasema Pastory Majani, mwalimu katika Shule ya Msingi Mugumu "B."



Mipango ya Serikali, inajumuisha ufundishaji wa walimu wote. Lakini inaelekea umuhimu umewekwa zaidi katika miundombinu na majengo.

Kuna faida gani kuwa na madarasa nadhifu wakati mwalimu anajiona hajaandaliwa kufundisha darasa lake?

Bila kuwapatia walimu mafunzo ya kutosha tunatarajiaje walimu hao wawe tayari kufundisha kama inavyotakiwa? Inavyoelekea uendelezaji wa nguvu kazi, moja ya malengo muhimu ya MMEM umewekwa kando.

Kubadilisha mtaala bila ya kuwaeleza walimu namna ya kufundisha masomo hayo mapya ni kama kujenga nyumba isiyokuwa na sebule. Kama walimu wamechanganyikiwa; ni dhahiri kwamba hata wanafunzi wao nao wamechanganyikiwa. Kuna haja kwa serikali kuandaa programu ya kueneza taarifa na mafunzo juu ya mtaala mpya na mbinu za kuufundisha mtaala huo.

3 Kwenda Shule Pamoja na Simba

Inaelekea kuna utata mkubwa kuhusu Elimu katika Wilaya ya Serengeti. Wananchi walidhani kwamba idadi ndogo ya wanafunzi wa darasa la kwanza na la pili, ilitokana na wazazi kutojali elimu. Lakini tulipowauliza baadhi ya wazazi huko, tuligundua kuwa ukweli ulikuwa tofauti kabisa. Tatizo halikuwa kwamba wazazi walikuwa hawataki watoto wao kwenda shule. Tatizo lilikuwa ni muda wa kuanza masomo na umbali wa shule.



Familia nyingi sehemu za Serengeti ni wakulima wafungaji ambao wanaishi pembezoni mwa Hifadhi za Taifa na Mbuga za Wanyama zilizofurika wanyama pori. Ili kufika shule inalazimu kutembea kupitia sehemu ambamo ni kawaida kukutana na kundi la nyati wakiwa malishoni au hata kumkurupusha tembo akipata mlo wake wa asubuhi. Kama shule inaanza saa 2 asubuhi, ina maana watoto lazima waondoke nyumbani majira ya saa 12.30. Huu ndio wakati mzuri hasa wa mawindo kwa wanyama wa mwituni. Wewe ungependa mwanao, mwenye umri wa miaka 7 apite katika pori lenye simba wanaowinda?

“Watoto hawa ni wadogo sana, hawawezi kumudu kutembea umbali wa kufika shule hata shule iliyo karibu kuliko zote, wakipitia katika mapori manene yenye wanyama wakali. Kwa sababu hatutaki kuona watoto wetu wakishambuliwa, tunaona ni afadhali tuwaache wakue kidogo kabla ya kuwapeleka shuleni, ili waweze kujilinda wenyewe,” anasema Mkongwe Babisi, mzazi kutoka Kijiji cha Mbalibali. Je hili ni ombi kubwa mno?

Katika Kijiji cha Mbalibali wanafunzi pia wanakabiliwa na tatizo la mafuriko ya mito katika msimu wa masika. Wazazi wanahofia kwamba, wakiwa na umri mdogo kama huo, watoto wao huenda wakafa maji wakati wakijaribu kuvuka mto. Kwa sababu hizo watoto hukaa nyumbani hadi mwisho wa masika.

Haya matatizo yanaweza kutatuliwa kwa jitihada kidogo. Mahudhurio ya watoto wa darasa la kwanza yanaendelea kupungua, na lazima ufumbuzi upatikane. Mzazi mmoja alipendekeza kwamba masomo ya darasa la kwanza na la pili yasianze mapema sana, ili watoto waweze kutembea kwenda shuleni kwa usalama. Pia kuna mazungumzo baina ya wanakijiji kuhusu kujenga madarasa rasmi kwa ajili ya madarasa ya chini karibu na kijiji ili watoto wadogo sana wasilazimike kutembea masafa marefu sana.

Kama tukichukuwa muda wa kusikiliza, huenda tukaelewa mashaka ya wazazi na jumuiya, badala ya kujengea dhana kuhusu dhamira na vitendo vyao. Labda tunahitaji kufanya uchunguzi wa kina ili tugundue mashaka halisi na ufumbuzi wake.

4 Fedha Zilizoahidiwa Hazifiki Shuleni

Kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM), idadi ya wanafunzi watakaoandikishwa katika shule za msingi itaongezeka sana. Lengo ni kwamba watoto wote wenye umri kati ya miaka 7 na 13 watakuwa shuleni ifikapo mwaka 2005. Ili kuzisaidia shule ziweze kuhimili huu mwongezeko mkubwa wa wanafunzi Serikali imeahidi kutoa ruzuku. Hii ina maana kwamba kila shule itapatiwa dola 10 za kimarekani kwa kila mtoto atakayeandikishwa. Awali ya hapo, dola 4 kati ya hizo itapelekwa katika ngazi ya Wilaya ili kununua vitabu na vifaa vinginevyo vya shule. Dola 6 zinazobaki zitapelekwa moja kwa moja shuleni.

Mwaka 2002, baadhi ya shule zilipokea shillingi 2000, kama dola 2, kwa kila mwanafunzi, lakini hazikupokea vitabu wala vifaa vingine. Mwaka 2003, pamoja na kuongezeka kwa uandikishaji, ruzuku kule Ukerewe haikufikia kiwango kilichokubalika. Tulipowauliza wakuu wa shule na wanakamati sababu, walijibu kwamba hawajui ni kiasi gani walipaswa kupokea.

Pesa zilitumwa, hakukuwa na barua ya kufafanua na kuthibitisha kiasi kilichotumwa. Kwa sababu wanakamati walikuwa na uelewa mdogo tu kuhusu kiasi gani kilitakiwa kulipwa hawakuona sababu ya kuhoji kiasi kilichopokelewa. Kama alivyosema Mwanakamati mmoja “Hatujui ni kiasi gani cha fedha tulichopaswa kupokea mwaka jana na tutakachopokea mwaka huu. Tunashukuru kwa msaada (ruzuku) huu, lakini ni vigumu kufanya mipango. Kwa hiyo sisi hungoja tu fedha ziingie benki, kisha tunangoja maelekezo.”

Ili Kamati za Shule zipate kuimarika na kutimiza wajibu wao ipasavyo, wanapaswa kupewa taarifa kikamilifu. Wanapaswa kujua kiasi gani cha fedha wategemee ili waweze kufanya mipango madhubuti; wanapaswa kupokea fedha zilizoahidiwa. Ni vigumu kujenga uwazi, demokrasia shuleni ikiwa baadhi ya viongozi wanashindwa kuwa mfano bora wenyewe.

5 Mbao za Matangazo Zasaidia

Kwa mara ya kwanza, katika Shule ya Msingi Nkilizya matokeo ya mitihani ya wanafunzi, yanabandikwa kwenye mbao za matangazo. Jambo hili limeleta msisimko wa aina yake. Wazazi ambao hapo awali waliepuka maeneo ya shule sasa wanakusanyika kuangalia maendeleo ya watoto wao. Walimu wana shauku kujua matokeo ya madarasa mengine. Wanafunzi wanabishana na kupinga nani atapata alama za juu zaidi.


Hata hivyo mbao za matangazo si kwa manufaa ya wazazi wenye udadisi na wanafunzi wenye ushindani. Dhana muhimu ya kuwepo kwa mbao hizo ni kufanya majadiliano ya wazi miongoni mwa wanafunzi, walimu na wanajamii. Inaelekea hili limetimia kwani tangu hizi mbao ziwekwe, zimekuwa zinafurika mashairi, mawazo, maoni.

“Tunaandika vitu kama mashairi na maoni yetu wenyewe na kuyabandika kwenye ubao, na tunashangaa kwani walimu wanayachukulia vizuri. Aidha, mbao za matangazo zimetumiwa kuwataarifu wanafunzi na wazazi kuhusu hali ya shule kimapato. Katika shule za msingi za Hamuyebe na Nakatunguru, taarifa kama makadirio ya mapato na matumizi ya shule, fedha zilizopokelewa, matumizi na salio hubandikwa kwenye ubao wa matangazo. “Kila yanapotokea mambo mapya, sisi huenda kwenye ubao wa matangazo na tunayaleta. Kwa mfano, ukienda pale sasa hivi, utakuta tangazo la taarifa ya mapato na matumizi ya shule yetu. Uwazi huu hujenga kuaminiana kati yetu na uongozi wa shule,” anasema Jesca Ochieng, mwanafunzi wa Shule ya Msingi ya Nakatunguru.

Ubao wa matangazo umethibitika kuwa njia rahisi ya kuwezesha majadiliano miongoni mwa wanafunzi, walimu, na jumuia na kujenga uwazi juu ya matumizi ya fedha za shule. Ni chanzo cha taarifa kwa wananchi wenye maswali. Unawapa watoto nafasi ya kusema na hata kutoa changamoto kwa viongozi. Juu ya yote wanafunzi, walimu na wazazi wamekuwa wakijihusisha na shule.

6 Elimu Bora Dhidi ya Mahari

"Katika mila zetu za Kikurya, taratibu za kimila bado zinathaminiwa na kupewa kipaumbele katika maisha yetu ya kila siku. Kijijini mwetu tunaigawa elimu katika makundi mawili: shule ya jumuiya na shule rasmi ya serikali. Shule ya Jumuia hulenga taratibu za kimila na utamaduni "kanuni za marika" kama vile ukeketaji unaojulikana kama Saro, kutahiri na ngoma ya kiasili inayopendwa sana iitwayo "litungu." Shule rasmi ya Serikali huhusisha madarasa rasmi, mitaala na vitabu," anasema Mzee Peter Mosama wa Kijiji cha Mbalibali.



Mara binti anapotimiza umri wa kukeketwa, wazazi hutumia fedha nyingi kumnunulia nguo na viatu, kumtayarisha kwa ndoa. Ni wakati muhimu sana katika maisha ya msichana, wakati unaostahili kuangaliwa sana. Shida ni kwamba, wazazi haohao ambao hutumia kiasi kikubwa cha fedha kuwatayarisha mabinti zao kuolewa, hudai hawana fedha za kununua vifaa vya shule, vitabu, sare na viatu.

Tulipowauliza wazazi katika Kijiji cha Mbalibali juu ya umuhimu wa Elimu, walisema kwamba mara nyingi Elimu ya Kijamii ndiyo hupewa kipaumbele. Wazazi wako tayari kutoa fedha nyingi ili watoto wao wa kike wakeketwe, kwa sababu wasichana waliotahiriwa kimila, hutolewa mahari kubwa zaidi. Lakini shule rasmi, kwa maoni ya wazazi walio wengi, hailipi chochote.

Wazazi wanashindwa kutambua kwamba binti zao pia wana haki na wanahitaji masomo rasmi. Kwa kweli watoto hawa wangepaswa wawe na haki ya kuchagua wenyewe. Lakini hata kama wangepewa fursa hiyo huenda wasingejitokeza kwa kuogopa kuwaudhi wazazi wao. Kinachohitajika ni majadiliano ya wazi na wanajamii, kuhusu faida za elimu rasmi kwa watoto wote, wasichana na wavulana.

Utafiti unaonyesha kwamba hatimaye, elimu rasmi inalipa. Elimu hii huchangia katika kuleta afya bora zaidi pamoja na ustawi, ajira bora na ushirikishwaji zaidi katika jumuiya. Madhara ya kiafya yatokanayo na ukeketaji na uhusiano wake na haki za wanawake pia yamedhihirika.


Swali ni je itawezekanaje kuwa na mazungumzo ya wazi kuhusu masuala haya? Je, tunawezaje kuheshimu na kudumisha mila na hapohapo kukuza elimu na haki za binadamu?

Kuna haja ya Wanazuoni kutafiti uwezekano wa kuziba pengo baina ya aina hizi mbili za elimu katika jamii ya Wakurya. Pengine njia muafaka inaweza kuchukua baadhi ya mila na kuziingiza katika elimu rasmi. Aidha, majaribio yanaweza kufanywa ili kuingiza mambo yanayofaa katika elimu rasmi na kuyachanganya katika elimu ya jamii. Jambo hili pengine huenda litawawezesha Wakurya kuona uhusiano na umhimu wa elimu rasmi na elimu ya kimila. Shule nazo zinaweza kukubalika zaidi katika jamii.

Ili kuwe na mabadiliko jamii inahitaji wasichana na wanawake kuwezeshwa na pia viongozi wenye mtazamo wa kimaendeleo.

7 Wazo la Mwalimu Labadili Shule

Kwa muda mrefu sana, Shule ya Msingi, Nkillizya haikuwa na jambo la kujivunia. Wengi wa wanafunzi wa darasa la saba (7) hawakufaulu mitihani yao na wanafunzi wawili au watatu tu, ndio waliochaguliwa kujiunga na shule za Sekondari kila mwaka; hii ikiwa ni moja ya idadi za chini kabisa mkoani. Walimu waliokatishwa tamaa waliamua kulishughulikia suala hili.



Walikutana ili kung'amua chanzo cha tatizo hili, na waligundua kwamba sababu ilikuwa ni wazi kabisa: wanafunzi walikuwa hawapati muda wa kutosha kukaa na walimu wao. Na hasa wanafunzi ambao walihitaji msaada wa ziada hawakupata muda wa kusikilizwa ili walingane na wenzao.

Walimu walikuja na wazo: walikubaliana kuwapa muda wa ziada wanafunzi wa darasa la 7 na 4. Lakini hili lingefanyika tu kama wazazi nao wangekuwa tayari kuchangia: ingewabidi watoe chakula kwa walimu.

Kamati ya shule iliafikiana na wazo hilo na kuchukua hatua mara moja kwa kuuarifu uongozi wa kijiji. Serikali ya kijiji iliitisha mkutano wa wanakijiji wote kujadili pendekezo lile. Wazazi wenye watoto shuleni walikubaliana kuchangia shilingi 50 kila mmoja kwa ajili ya chakula cha walimu.

Mnamo 2002, idadi kubwa ya wanafunzi wa darasa la 7 walifaulu mitihani na kupata alama zilizovuka kiwango cha kawaida, na wanafunzi 10 walichaguliwa kwenda shule za sekondari.

Matokeo haya yalistaajabisha na kuleta changamoto: Watu walihamasika na hali mpya ya kujiamini ilisambaa na kuenea miongoni mwa jamii. Kila mtu kijijini alisherehekea matokeo mazuri, na wakawa na shauku ya kuhakikisha kuwa wanapata mafanikio zaidi katika mwaka uliofuata, yaani 2003.


Kila mtu amehamasishwa na matokeo hayo. Walimu wamepata changamoto ya kuongeza ubora wa matokeo. Wanafunzi wamehamasika kufanya vizuri. Wanajamii wamegundua kwamba juhudi zao za pamoja zinalipa. Baadhi ya wazazi kwa ridhaa yao wenyewe wameamua kuongeza michango yao. Kwa mara ya kwanza kabisa wazazi wanajisikia kwamba kweli wanahusika katika shule ya watoto wao, siyo watazamaji wasio na kauli katika mambo yanayoendelea.

Hili inaonesha kwamba wana jumuiya wanathamini kufaulu kwa watoto wao. Wanachohitaji ni fursa ya kushiriki na kuleta mabadiliko.

8 Majalada Yapotea Siku ya Malipo

Walimu katika Wilaya ya Serengeti wameonyesha masikitiko yao kuhusu kushindwa kupata mishahara katika muda uliowekwa. Baadhi ya walimu wamesema kwamba, katika siku ya malipo hulazimika kukatisha masomo na kwenda katika Ofisi ya Wilaya, na wakifika huko huambiwa majalada yao yamepotea, na wanaporudi shuleni, wanafunzi wote huwa wameondoka na siku imepotea.

“Unaweza kwenda leo ukakuta jalada lako juu ya meza, na watakuahidi kuwa ukija baada ya siku tatu kila kitu kitakuwa tayari. Lakini ukienda utaambiwa jalada limepotea. Je, unaweza kuliamini hili?” aliuliza mwalimu kutoka Shule ya Msingi Buruga.




Siku ya malipo haina tarehe maalumu, na walimu hawajulishwi kuwa mshahara umefika wakachukue. Wanasafiri umbali wa kilomita 30 au zaidi wakidhani ni siku ya malipo. Hurudi mikono mitupu, wakati watumishi wengine Wilayani tayari huwa wamelipwa mishahara yao. Bila shaka kuna tatizo hapa.

Ukosefu huu wa maadili ya kitaaluma kwa upande wa baadhi ya watumishi wa Umma Wilayani haukubaliki; na unaathiri ufanisi wa walimu na wanafunzi. Wanafunzi hukosa muda muhimu sana wa masomo na walimu wanalazimika kufanya biashara ndogondogo ili kulisha familia zao. Ndiyo maana hawawi makini darasani.

Watumishi wa Umma Wilayani wana jukumu la kuwataarifu walimu wakati mishahara inapokaribia kufika na ikifika walipwe ipasavyo. Je, upatikanaji wa elimu bora kwa wote utawezekanaje wakati walimu hawana uhakika wa hali yao kiuchumi?

9 Wanafunzi Hutaka Kuzijua Kanuni tu

Ingawa kumekuwa na vilio kutoka kwa wanaharakati kuhusu sheria ya viboko, suala sio wanafunzi kupinga utaratibu huo, bali hutaka kujua haki zao ili waweze kuwauliza walimu wao kama wakidhani hawatendewi haki.



“Viboko visifutwe mashuleni kwa sababu sisi wanafunzi ni wasumbufu. Kama hakuna viboko hali itakuwa mbaya zaidi. Wanafunzi hawatawaheshimu walimu kwa sababu wanajua walimu hawatawafanya lolote. Tatizo ni namna ya kulisimamia. Mathalan kukiwa na walimu watano kila mmoja na idadi yake ya fimbo za kumchapa sehemu yoyote atakanayo, unafikiri nini kitatokea kwa mwanafunzi yule?” anauliza Maishufa Abdallah mwanafunzi wa Shule ya Msingi Mapinduzi.

Wanafunzi si wajinga. Wanajua kwamba nidhamu inaweza kuvuka kiwango na wanataka kujua walimu wanaruhusiwa kuchapa wapi, wanaruhusiwa kuchapa wanafunzi viboko vingapi na kwa kosa lipi. Kwa namna hiyo, kila mtu anajua mipaka yake.

Baadhi ya wanafunzi walisema kwamba viboko viruhusiwe madarasani kwa sababu inayoeleweka, wanafunzi watiwe moyo ili wachangie darasani, lakini wanafunzi wengi wanaogopa kuchangia darasani kwa sababu wanajua walimu huwachapa wale wanaotoa majibu yasiyo sahihi. Viboko viwe kwa wale wanaovunja sheria za shule na si kwa watoto wanaotaka kuchangia darasani.

Wanafunzi wameshauri viboko vifutwe kwa watoto wa darasa la kwanza na la pili. Sio vizuri kuwapa adhabu ya viboko watoto wadogo kwa sababu inawakatisha tamaa ya kwenda shule.

Mjadala juu ya adhabu ya viboko mashuleni ihusishe wanafunzi wenyewe, wanafunzi wana mawazo mazuri ya kuchangia katika masuala haya. Ni lazima tuwasikilize na kuwapa changamoto pia tuwajumuishe wanafunzi katika mchakato wa maamuzi, kinyume na kuamua kwa niaba yao. Inawezekana kuwa na nidhamu bila adhabu ya viboko. Je utaratibu mwingine ni mbaya zaidi ya kuchapa? Je ni sawa kuchapa hata kama ni sawa? Au kuchapa ni kitu kibaya siku zote? Tuanze mjadala.

10 Maktaba Zachochea Kujifunza

Kwa mujibu wa Wanafunzi na Walimu kutoka Wilaya ya Ukerewe, ongezeko la maktaba katika shule za msingi linaleta tofauti inayoonekana katika maendeleo ya wanafunzi. Katika mtihani wa majaribio mwaka huu, wanafunzi nane (8) kati ya kumi (10) waliofaulu vizuri hutoka katika shule zenye maktaba. Watu wengi wameonyesha matumaini kwamba maktaba ni chombo muhimu katika jitihada za kuinua kiwango cha Elimu Tanzania.



Walimu pia huona umuhimu wa maktaba kwa tafiti zao. Mpaka sasa wanafunzi wamekuwa wakiwategemea zaidi walimu wakiwa darasani, hata hivyo walimu hawana vifaa kwa ajili ya kuendesha vipindi vyenye mvuto na changamoto kwa wanafunzi.

Shule zenye maktaba zina madarasa yenye maendeleo kwani walimu huwatia moyo wanafunzi na wanafunzi pia huwachangamsha walimu kwa maoni yao.

“ Kutumia maktaba wakati mwingine hukufanya uwe mbele ya mwalimu, kwa sababu kwenye maktaba, unaweza kukaa na kujisomea kwa utulivu huku ukinukuu mambo muhimu kwa umakini zaidi,” alisema mwanafunzi mmoja.


Lakini licha ya faida dhahiri za maktaba kwa walimu na wanafunzi, inaelekea uanzishwaji wa maktaba si kipaumbele kwenye Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (MMEM). Shirika la “CARE International” limefadhili jumla ya maktaba za shule 62 katika Wilaya ya Ukerewe, chini ya mpango wa “Tusome Vitabu.”

Maktaba hizi hujumuisha vitabu pamoja na vifaa vinginevyo vya mafunzo. Vitabu vingi vya watoto husaidia kuchangamsha uwezo wa watoto kuwaza. Kama Mwalimu mmoja alivyosema “ni kama chemchem ya maji katika jangwa. Wanafunzi wangu wanaweza kuitumia kutuliza kiu ya kujifunza.”

Maktaba kama zile zinazofadhiliwa na mpango wa “Tusome Vitabu” zinaweza kupatikana katika shule katika baadhi ya wilaya. Swali ni: Je Serikali na wananchi wapo tayari kulifanya lengo la kuanzisha maktaba hizi katika kila shule nchini litimilke? Je moyo na hamasa hiyo vitaweza kuenezwa nchi nzima?

11 Kutoa Majibu Yasiyo sahihi kwa Makusudi

Baadhi ya Wazazi katika Wilaya ya Serengeti wamekuwa wakiwakatisha tamaa watoto wao kushinda katika mtihani wa darasa la saba, kwa kuwalazimisha kuandika majibu yasiyo sahihi kwenye mitihani yao. Wazazi hao huwatishia watoto wakiwatahadharisha kwamba wasipofuata wasemayo, "watalaaniwa." Wengine huwaambia watoto wao kuchagua kati ya wazazi na elimu. Kama kawaida watoto huogopa kwenda kinyume na matakwa ya wazazi wao. Kitu gani kinatokea?



Majadiliano kati ya wazazi na wanafunzi ulionyesha kwamba wazazi hawataki watoto wao wachaguliwe kwenda Sekondari kwa sababu hawana fedha za kulipia gharama zote. Lakini wanafunzi hawakubali mtazamo huu na kusema wazazi wao wanao uwezo wa kutosha kulipia shule.

Mzee Peter wa Kijiji cha Mbalibali alitupa mwanga juu ya suala hili. "Sisi huthamini ng'ombe kuliko elimu. Kwa kumuoza mtoto wa kike, una uhakika

wa kuongeza idadi ya ng'ombe wako na hivyo kupata umaarufu kijijini. Mtoto wa kike akiendelea na elimu ya Sekondari inamaanisha ng'ombe watapatikana baadaye sana katika familia hiyo."


Maelezo haya yanasaidia kuelezea kwa nini idadi ya wanawake wanaoandikishwa ni ndogo sana. Jamii ya Serengeti bado inaamini utamaduni wa kukeketa, ndoa za utotoni na masuala mengine yanayoathiri maendeleo ya watoto wa kike kielimu.

Ingawa ni vizuri kuenzi na kuheshimu utamaduni wetu, sera za Serikali ziko wazi kwamba watoto wote wana haki ya Elimu ya Msingi. Watoto wawe na uwezo wa kuchagua wenyewe ni majibu ya aina gani waandike katika mitihani yao. Lakini wanahitaji msaada na uelewa wa wazazi wao. Mabadiliko ya kweli lazima yaanzie nyumbani na katika jamii.

Katika kuleta mabadiliko haya, asasi zisizokuwa za kiserikali, taasisi za kijamii pamoja na vikundi vya wanawake, walimu na viongozi wa jamii, wanahitaji kufikisha ujumbe huu kwa jamii na kuanzisha mijadala. Wanajamii, watoto na wakubwa watafute njia bora zaidi ya kuheshimu utamaduni, angalau sehemu ya mila hizo. Serikali ina mchango wa kutoa, kutoa elimu bora ambayo itajenga ujuzi na kujiamini ili wahitimu wawe wanawezeshwa kweli.

12 Mwanafunzi Atia Saini Kwenye Hundi za Shule

Shule ya msingi Mugumu 'B' katika Wilaya ya Serengeti imepiga hatua kubwa katika suala la demokrasia na uwazi katika shule. Farida Sostenus wa miaka 13 amekuwa mwanafunzi wa kwanza kuhusishwa katika utawala wa fedha za shule. Wajumbe wa Kamati ya Shule wamechaguliwa kidemokrasia na alipewa jukumu la kuwa mmoja wa wapiga saini katika akaunti ya shule. Katibu wa kamati ya shule na mwalimu mkuu Bwana Venance Mathew wamefurahishwa sana. Amesema ni wakati muafaka kwa wanafunzi kuhusishwa katika uongozi wa shule yao. Hata hivyo, fedha hizo ni kwa ajili yao.



Katika mkutano wa kamati ya shule, wajumbe walijadili juu ya kuwashirikisha wanafunzi katika uongozi wa fedha za shule ili kujenga uaminifu na uwazi.

"Tumeamua kuwa watia saini lazima wawe wale wanaowakilisha katika kamati ya shule yaani wanafunzi, walimu, wazazi na wazee wa kijiji," alisema.

Farida amesema kwamba amepewa mafunzo ya uongozi wa fedha na anajiamini katika nafasi yake. "Hakuna anayeweza kunidanganya juu ya mapato na

matumizi ya shule, ninao uwezo wa kuchambua bajeti ya shule na kupitia matumizi na mapato ya shule. Anaongeza kwamba anashukuru kwamba walimu na kamati ya shule wanamuheshimu. Wanasikiliza maoni yake na kukubaliana na haki zake.

“Hivi sasa ninahusika na uongozi wa fedha za shule, wenzangu wananiamini. Lazima nihakikishe kwamba wanajulishwa juu ya matumizi katika kuinua kiwango cha elimu katika shule yetu,” alisema Farida.

Kuwashirikisha wanafunzi katika eneo hili ni njia mojawapo ya kuboresha shule zetu. Inaonyesha jinsi wanafunzi wanavyoweza kuleta tofauti kama wakipewa nafasi na msaada. Bwana Mathew, Farida na wanakamati wa shule ya msingi Mugumu ‘B’ wawe mfano kwetu sisi sote.